JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO

# 2025



# DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2025

*Tume ya Mipango*

YALIYOMO

DIBAJI........................................................v

UTANGULIZI........................................................ix

1.0 DIRA YA MAENDELEO........................................1

1.1 Dhana ya Dira........................................1
1.2 Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025........2
*1.2.1 Maisha Bora na mazuri ........................3*
*1.2.2 Amani, Utulivu na Umoja ........................4*
*1.2.3 Utawala na Uongozi Bora ........................4*
*1.2.4 Jamii iliyoelimika na inayopenda kuifunza zaidi........................4*
*1.2.5 Uchumi Imara wenye Kuhimili Ushindani........................6*

2.0 MWELEKEO NA KASORO KATIKA DIRA ZA AWALI........................................7

2.1 Dira za Awali Nchini Tanzania........................7
2.2 Kasoro na Vikwazo........................................8
*2.2.1 Hulka tegemezi na fikra zilizodumaa kimaendeleo........................9*
*2.2.2 Uchumi dhaifu na Uwezo mdogo wa usimamizi wa uchumi........................11*
*2.2.3 Udhaifu katika Utawala na usimamizi wa Maendeleo........................12*
*2.2.4 Utamaduni Mbovu wa Utekelezaji.13*

3.0 MALENGO YA DIRA ..................................................14
3.1 Maisha Bora na mazuri ....................................14
3.2 Uongozi bora na utawala wa kisheria..............15
3.3 Uchumi Imara na wenye uwezo wa ushindani.......................................................16

4.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA KATIKA UTEKELEZAJI...........................................................18
4.1 Fikra za kimaendeleo na Utamaduni wa Kujitegemea.......................................................20
4.2 Ustadi na Uwezo wa Ushindani Kiuchumi........23
4.3 Uongozi bora na utawala wa kisheria...............27

5.0 UTEKELEZAJI WA DIRA...........................................30

6.0 HITIMISHO..................................................................37

# DIBAJI

Tumesimama mlangoni mwa karne ya 21, karne ambayo kwa vile itakuwa ya ushindani ni dhahiri itatawaliwa na wale wenye uwezo mkubwa kiteknolojia, tija kubwa katika uzalishaji, miundombinu imara na ya kisasa ya mawasiliano na uchukuzi na ya zaidi ya yote, nguvu kazi yenye ustadi mkubwa na hulka ya kujituma. Kama Taifa, tunawajibika kutafuta mbinu za kujirekebisha na kujiimarisha katika maeneo yote haya ili tuwe washiriki kamilifu, na si wasindikizaji tu, katika maendeleo ya dunia ya karne ya 21.

Katika kutafakari changamoto hii, wananchi wakiongozwa na Serikali yao, waliona umuhimu wa kuandaa Dira Mpya ya Maendeleo ya Taifa itakayoongoza harakati za maendeleo ya uchumi na jamii hadi mwaka 2025. Madhumuni ya Dira hii ni kuamsha, kuunganisha na kuelekeza juhudi na fikra zetu na rasilimali za Taifa letu katika maeneo ya msingi yatakayotuwezesha kufikia malengo yetu ya maendeleo, na kustahimili ushindani mkubwa wa kiuchumi ulio mbele yetu.

Dira hii haina budi kuungwa mkono na wananchi wote. Ndiyo maana katika kuiandaa tulitafuta maoni na ridhaa ya wananchi wengi kutoka sehemu zote za jamii yetu. Rasimu ya Dira ilijadiliwa na makundi mbali mbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, vyama vyote vya siasa, viongozi wa madhehebu mbali mbali ya dini, jumuiya za kina mama na vijana, vyama vya wafanyabiashara na wenye viwanda, wakulima, wasomi, watu

mashuhuri katika historia ya nchi yetu, na wananchi wa kawaida. Dira ya Maendeleo 2025 iliyoandikwa kwa utaratibu huu ni nguzo muhimu katika kujenga umoja na mshikamano wa kitaifa unaohitajika ili kuleta maendeleo katika hali ya amani, usalama, na uzalendo.

Dira hii pia imeandaliwa kwa kuzingatia tathmini ya kina ya historia na mwelekeo wa nchi yetu. Imetupa fursa ya kuelewa vyema tulikotoka, tulipo na kule tuendako. Uchambuzi umefanywa juu ya siasa na sera zetu, na mfumo wa utayarishaji mipango ya maendeleo na utekelezaji wake. Tumejifunza kutokana na ufanisi au mapungufu katika harakati hizo. Dira ya Maendeleo 2025 imebainisha mazingira muafaka yanayohitajika kuliwezesha Taifa letu kustawi kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Imebashiri mabadiliko na mwelekeo wa dunia kwa siku zijazo. Hivyo, katika utekelezaji, hatuna budi kuzingatia nafasi ya Tanzania katika dunia na wajibu wetu wa kukabiliana na mabadiliko yoyote yajayo kwa kujituma zaidi kwa juhudi na maarifa katika kazi zetu, na kuzitumia ipasavyo fursa na rasilimali nyingi ambazo nchi yetu inazo.

Mwanzo wa mafanikio katika jambo lolote ni dhamira na nidhamu katika kupanga na kutekeleza. Kwa kukubaliana juu ya Dira hii, tumetoa tamko la dhamira yetu ya kujinasua kutoka katika lindi la umasikini. Hivyo, kazi iliyo mbele yetu sasa ni kila mmoja kwa nafasi yake kuona na kutekeleza wajibu wake katika kutekeleza malengo tuliyojiwekea. Wizara na taasisi nyingine za Serikali, sekta binafsi, taasisi zisizo za kiserikali, jumuiya za

wananchi, vyama vya ushirika, vijiji, na makundi yeyote ya jamii yajielekeze katika kuchangia utekelezaji wa malengo ya Dira hii.

Amani, utulivu na usalama wa raia na mali zao ni mazingira ya lazima kabisa na ya msingi kwa maendeleo. Bila mazingira hayo Dira hii haitakuwa na maana, na wala hatutapata maendeleo. Hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu, kuepuka kila linaloweza kuwagawa Watanzania kama vile kubaguana kwa msingi wa dini, kabila, rangi, jinsia au eneo analotoka mtu. Ni wajibu wa kila mmoja wetu pia kumtenga na kumsuta yeyote anayeleta, kushabikia, au kuleta dharau, mifarakano, chuki na kutoaminiana katika nchi yetu. Nina imani kuwa Watanzania walio wengi ni wazalendo na waadilifu na wako tayari kuungana kupiga vita kasoro hizo.

Nina uhakika kwamba, kwa mshikamano tulionao kama Taifa, tutafanikiwa kutekeleza Dira hii. Linalowezekana leo lisingoje kesho.

Mungu ibariki Tanzania na tujalie nguvu ya kutekeleza Dira yetu.

BENJAMIN WILLIAM MKAPA
**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# UTANGULIZI

Haja ya kuwa na Dira ya Maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Tanzania ni matokeo ya hatua zilizochukuliwa kurekebisha uchumi na hasa zile zilizokuwa na mwelekeo wa kurekebisha mfumo wa uchumi zilizoanza katikati ya mwaka 1986. Hatua hizi za kufanya marekebisho ya kiuchumi na kijamii zilitokana na matatizo ya kiuchumi yaliyoikumba nchi yetu pamoja na dunia kwa jumla kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1980. Pili, serikali ilibaini kwamba sera na mikakati ya kiuchumi ya hapo awali ilikuwa haiendani na mwenendo wa dhana ya soko la maendeleo ya teknolojia yaliyokuwa yakitokea ulimwenguni, na kwa hiyo serikali ilianza kuandaa programu za miaka mitatu mitatu za kurekebisha uchumi ambazo kwa jumla mikakati ilielekeza nguvu katika kutatua baadhi tu ya masuala ya kiuchumi na kijamii, na maeneo ya msisitizo yakiwa yanabadilika mara kwa mara. Programu hizo za kuleta marekebisho ya kiuchumi, zimetuchukua muda mrefu – karibu miaka kumi na mitano. Katika kipindi hiki kirefu, dhana nzima ya kuleta maendeleo ya nchi na wananchi wake ikawa inaanza kupotea na kwa hiyo nchi ikakosa mwelekeo wa malengo ya maendeleo ya muda mrefu. Serikali na wananchi kwa jumla walibaini kasoro hii ya kutokuwa na mwelekeo wala falsafa ya maendeleo ya muda mrefu. Dira ya Maendeleo 2025 inaziba pengo hili.

Serikali ilianza zoezi la kuandaa Dira hii mwaka 1995. Timu ya Wataalamu walioteuliwa kutoka sehemu mbali mbali za jamii ilikuwa ndiyo kitovu cha zoezi hili chini ya usimamizi wa Tume ya Mipango. Ili kufikia muafaka wa kitaifa katika malengo ya Dira, suala la ushirikishwaji wa wananchi lilihimizwa tangu hatua za mwanzo za utayarishaji. Ushirikishwaji wa wananchi ulifanyika kwa njia mbali mbali zikiwemo kongamano, mahojiano na watu mbali mbali, na mikutano iliyohusisha makundi mbali mbali katika jamii. Pia vyombo vya habari vilitumika, ikiwa ni pamoja na makala katika magazeti na midahalo katika redio na televisheni.

Mambo ya msingi katika Dira hii yamefafanuliwa katika maeneo makuu sita. Kwanza ni ufafanuzi wa dhana na upeo wa Dira ya Maendeleo. Sehemu hii inaeleza sifa za nchi yetu zinazotarajiwa kuwepo ifikapo mwaka 2025 ikiwa ni pamoja na wananchi kuwa na maisha bora na mazuri; amani, utulivu na umoja; utawala na uongozi bora; jamii iliyoelimika na inayojituma katika masuala ya maendeleo; na uchumi wenye uwezo wa ushindani na wenye ukuaji wa kudumu kwa maslahi ya watu wote.

Sehemu ya pili inachambua kwa kifupi mwelekeo wa Dira za awali tangu Taifa letu lipate uhuru. Uchambuzi huu unaonyesha mafanikio na matatizo yaliyojitokeza kiasi cha kudhihirisha haja ya kuwa na Dira mpya ya maendeleo.

Malengo makuu matatu ya Dira ya Maendeleo 2025 – ambayo ni: kuwaleta wananchi maisha bora na mazuri; uongozi bora na utawala wa sheria; na kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani – yameelezwa kwa undani katika sehemu ya tatu. Malengo haya siyo tu yanajumuisha masuala ya uchumi bali pia masuala yote ikiwa ni pamoja na masuala ya kijamii kama vile elimu, afya, mazingira, kuinua ushiriki wa wananchi katika kujiletea maendeleo yao wenyewe, n.k. Msukumo wa malengo haya ni kuwa na maendeleo ya wananchi yaliyo endelevu.

Sehemu ya nne inahusu mambo muhimu yanayohitaji kuzingatiwa katika utekelezaji wa malengo ya Dira. Sehemu hii inabainisha mambo ambayo jamii kwa jumla haina budi kuyazingatia ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Dira unafanikiwa. Mambo au nguzo hizo za utekelezaji ni pamoja na wananchi kujenga fikra za ushindani wa kimaendeleo na utamaduni wa kujitegemea.

Sehemu ya tano inatoa maelekezo ya msingi kuhusu utekelezaji wa Dira ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kufanya mapitio na marekebisho ya sheria na mifumo ya taasisi mbali mbali nchini ili kuona kama inakidhi mahitaji ya utekelezaji wa Dira hii. Pia ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kutekeleza programu za maendeleo yao wenyewe umesisitizwa, ikiwa ni pamoja na kuwa na mfumo sahihi wa kuratibu na kutathmini utekelezaji wa Dira. Inasisitizwa kwamba ni kwa njia hii tu ya ushirikishwaji ndipo Dira inazingatia maendeleo ya watu na

kusimamiwa na watu wenyewe, mambo ambayo ni ya msingi katika kuwafanya wananchi wawe na wajibu katika kufanikisha malengo yao.

Mwisho, ninaamini kwamba ikiwa tutaweza kuzingatia mambo yote muhimu yaliyoainishwa katika Dira hii, Taifa letu litakuwa limepiga hatua kubwa sana katika kuongeza ari ya maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa maisha ya wananchi kwa jumla. Ningependa kuchukua nafasi hii kuwashukuru Watalaam na wananchi walishiriki katika kuandaa Dira hii. Pia ningependa kuwashukuru Wahisani kutoka nje waliotoa misaada ya kifedha na mingineyo katika kufanikisha zoezi hili, hasa Shirika la Kimataifa la Maendeleo (UNDP), Serikali ya Japan, na Umoja wa Nchi za Ulaya (European Union) na Serikali ya Ireland.

Ni matumaini yangu kwamba hawa na wengine wengi wataendelea kushirikiana nasi katika hatua ya utekelezaji; hususan kwa kutuunga mkono kwa hali na mali katika kutekeleza vipaumbele vitakavyoainishwa kitaifa kutuelekeza kwenye malengo ya Dira.

NASSORO WAMCHILOWA MALOCHO (MB)
Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Mipango na
Makamu Mwenyekiti
**TUME YA MIPANGO**

# 1.0 DIRA YA MAENDELEO

## 1.1 Dhana ya Dira

Mnamo miaka ya kati ya 1980, Serikali ilibaini kuwa sera na mikakati ya awali ya maendeleo ilikuwa haiendi sambamba na mwenendo wa dhana ya soko na maendeleo ya teknolojia yaliyokuwa yakitokea katika nchi za jirani na ulimwengu kwa jumla na pia hazikuzingatia mabadiliko halisi yaliyokuwa yakitokea nchini katika mazingira ya kijamii na kiuchumi.

Hivyo, kuanzia katikati ya mwaka 1986, Serikali ilianza kufanya marekebisho ya kijamii na kiuchumi ambayo yanaendelea kutekelezwa hadi sasa. Hata hivyo, Serikali na wananchi kwa jumla wamebaini kwamba marekebisho hayo ya kijamii na kiuchumi hayakuwa yakiongozwa na mwelekeo wala falsafa ya maendeleo ya muda mrefu.

Kutokana na haja ya kuwa na maendeleo yanayotokana na falsafa thabiti na yanayoongozwa na wananchi wenyewe ndipo wazo la DIRA ya maendeleo ya muda mrefu lilipojitokeza. Aidha, haja hiyo ilisisitizwa na azma ya Serikali ya kuamsha matumaini na uzalendo wa wananchi.

Dira ya Maendeleo ni kielelezo ambacho kwacho jamii au taifa linaongozwa kufanikisha "matakwa" au matumaini ya

kuwa na maisha bora (zaidi) katika muda unaokusudiwa na matakwa hayo sharti yaeleweke na kukubaliwa na jamii au taifa linalohusika.

## 1.2 Dira ya Maendeleo ya Tanzania – 2025

Mtanzania atakayezaliwa leo atakuwa ni mtu mzima, atakuwa amejiunga na kundi la wafanyakazi, na labda atakuwa ameanza kuwa mzazi ifikapo mwaka 2025. Hali kadhalika, Mtanzania ambaye ameanza kufanya kazi hivi karibuni atakuwa anajiandaa kustaafu ifikapo mwaka 2025. Je! Ni jamii ya aina gani itakayokuwa imejengeka ifikapo mwaka 2025? Kinachotarajiwa ni kuwa jamii ambayo watanzania hawa watakuwa wakiishi wakati huo itakuwa ni yenye maendeleo ya kuridhisha na maisha bora. Umasikini uliokithiri utaondoka na kubaki kuwa jambo la kihistoria. Kwa maneno mengine, inategemewa kwamba Watanzania watakuwa wamejikomboa kutoka katika kundi la nchi maskini na kuweza kuingia katika kundi la nchi zenye viwango vya kati vya mapato na hali bora ya maisha ifikapo mwaka 2025. Uchumi utakuwa umebadilika kutoka uchumi unaotegemea kilimo chenye tija ndogo na badala yake kuwa na uchumi wenye kuongozwa na sekta ya viwanda na kilimo cha kisasa chenye tija kubwa na kinachohusiana kwa karibu na maendeleo ya viwanda na sekta za huduma mijini na vijijini. Katika hali hiyo msingi madhubuti wenye uwezo wa kuhimili vishindo vya ushindani na wenye tija ya hali ya juu utakuwa umejengeka. Kulingana na matarajio hayo, Tanzania ya mwaka

2025 inatazamiwa kuwa ni Taifa lenye sifa kuu tano zifuatazo:-

- *Maisha bora na mazuri;*
- *Amani, utulivu na umoja;*
- *Utawala na uongozi bora;*
- *Jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi; na*
- *Uchumi wenye uwezo wa ushindani na kujiletea ukuaji wa kudumu kwa maslahi ya watu wote.*

### *1.2.1 Maisha Bora na mazuri*

Kimsingi maendeleo ya Taifa hayana budi yamlenge binadamu, yatokane na ukuaji endelevu wa uchumi, yahusishe watu wote na yatokomeze umaskini uliokithiri. Maendeleo haya kwa Tanzania yana maana ya kuwa na mfumo wa uzalishaji na mgawanyo wa mapato wenye misingi ya usawa na usiokuwa na aina yoyote ya vizuizi kijamii na kisiasa vinavyoupunguzia umma (wanaume, wanawake, wavulana, wasichana, vijana na wazee, walemavu na wasio walemavu) haki zake za kidemokrasia na kushiriki mambo mbali mbali katika jamii. Kwa maana hiyo, ifikapo mwaka 2025, tofauti za rangi na kijinsia zitakuwa zimefutika na hivyo harakati za kiuchumi kutokuendeshwa kwa misingi ya rangi au jinsia. Mahusiano yote ya kijamii na taratibu zenye kulea na kuendeleza tofauti katika makundi mbalimbali ya kijamii (k.mv./sheria, mfumo wa kisiasa, taratibu za ajira, elimu na mila) zitakuwa zimeondolewa kabisa.

### *1.2.2 Amani, Utulivu na Umoja*

Taifa ni sharti lifaidi amani, utulivu wa kisiasa, umoja wa kitaifa na mshikamano wa kijamii ndani ya mazingira ya kidemokrasia na uvumilivu wa kisiasa na kijamii. Ijapokuwa kwa muda mrefu Tanzania imebahatika na kuwepo kwa umoja wa kitaifa, amani na utulivu, juhudi za makusudi hazina budi kuchukuliwa ili kukuza, kulea na kuendeleza mambo hayo kama mihimili muhimu kwa mafanikio ya Dira.

### *1.2.3 Utawala na Uongozi Bora*

Tanzania inathamini uongozi bora na utawala wa kisheria katika harakati za uzalishaji mali na mgawanyo wa mapato siku zote na hujitahidi kuhakikisha kwamba watu wake wana uwezo wa kuwawajibisha viongozi wake na watumishi wa umma. Ifikapo mwaka 2025, utawala na uongozi bora utakuwa umeota mizizi ndani ya jamii yetu na hivyo kujenga utamaduni wa uwajibikaji, kuenzi na kuzawadia utendaji mzuri na kupiga vita rushwa na maovu mengine katika jamii.

### *1.2.4 Jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza zaidi*

Tanzania imedhamiria kuwa Taifa ambalo watu wake watakuwa na fikra za kimaendeleo na ari ya kiushindani. Sifa hizi zinatokana na misingi madhubuti ya elimu na maarifa na ni muhimu katika kuliwezesha Taifa kutumia rasilimali zake za

ndani kwa ufanisi mkubwa na kuweza kuwapatia watu wake mahitaji ya msingi na kuweza kujenga msingi madhubuti wa ushindani kiuchumi, kikanda na dunia kwa ujumla. Tanzania sharti ijizatiti kuweza kujenga ubunifu, ustadi na elimu bora ili kuweza kukabiliana vyema na changamoto za kimaendeleo na kuweza kushindana kikamilifu kikanda na kimataifa, kwa kuelewa ukweli kwamba uwezo wa kushindana katika karne ya 21 utatokana na viwango bora vya elimu na maarifa.

Kwa madhumuni ya kuyafikia hayo, Tanzania haina budi:

- Ijijengee misingi ya kujitegemea inayotokana na mazingira ya ukombozi wa kisaikolojia, kifikra na kuweza kujiamini ili jamii iweze kuamua na kuliongoza gurudumu lake la maendeleo kwa lengo la kutosheleza mahitaji ya msingi ya watu wote, wanaume, wanaweke na watoto.

- Liwe ni taifa ambalo watu wake wana fikra na mila zenye kuthamini maendeleo ya watu yanayotokana na juhudi za kufanya kazi, utaalamu, ustadi wa kibiashara, ubunifu, uvumbuzi na uadilifu na wawe ni watu wenye kujiamini na wenye kuheshimu watu wa jinsia zote. Watu wake hawana budi wajijengee umoja wa kujamii lakini bila kufifisha juhudi na ubunifu wa kibinafsi.

- Liwe Taifa lenye viwango vya juu kielimu katika ngazi zote. Liwe ni Taifa lenye kutoa idadi ya kutosha ya

wataalamu wenye ujuzi, maarifa na uwezo wa kuyatatua matatizo ya kijamii, na kuiwezesha jamii kukabiliana na changamoto za kimaendeleo na kujijengea uwezo wa kuhimili ushindani katika ngazi za kikanda na kimataifa.

### *1.2.5 Uchumi Imara wenye kuhimili Ushindani*

Tanzania haina budi iwe imejijengea uchumi wenye misingi imara na wenye uwezo wa ushindani ili jamii iweze kukabiliana na changamoto za maendeleo na kuweza kwenda sambamba na mabadiliko ya masoko na teknolojia katika kanda na ulimwenguni kwa jumla.

## 2.0 MWELEKEO NA KASORO KATIKA DIRA ZA AWALI

### 2.1 Dira za Awali Nchini Tanzania

Tanzania imepitia katika Dira mbili za Maendeleo ya Taifa: kwanza, ni Dira ya kujipatia Uhuru. Kila Mtanzania alilielewa na kuliafiki lengo hilo, ambalo msingi wake ni haki za binadamu. Hata hivyo, mara baada ya kupata uhuru, ilibainika kuwa sio watu wote walioelewa wajibu wao katika nchi iliyo huru, kwamba ili kufaidika na uhuru huo iliwajibika kila mmoja afanye kazi kwa kujituma. Hivyo, mara baada ya uhuru ikaanzishwa kampeni ya "Uhuru na Kazi". Kampeni hii ilikuwa na lengo la kuwakumbusha watu juu ya wajibu wao na umuhimu wa kufanya kazi kwa uhodari ili kuweza kupata maendeleo yaliyokusudiwa wakati wa mapambano ya kutafuta uhuru.

Dira ya pili ilikuwa ni ile ya Azimio la Arusha. Azimio lilifafanua falsafa ya ukombozi wa kiuchumi na kijamii chini ya misingi ya ujamaa na kujitegemea kama lengo la muda mrefu kwa Watanzania. Azimio hili lilipokelewa na kukubalika na Watanzania walio wengi na kuwahamasisha katika utekelezaji wake. Kwa hiyo kuanzia Februari 1967, Dira ya Maendeleo ya Tanzania sawia na sera za mageuzi ya kijamii na kiuchumi zikawa zikiongozwa kwa misingi na programu za Azimio la Arusha.

Inaeleweka, hata hivyo, kwamba mikakati ya utekelezaji wa Azimio la Arusha haikuzingatia kikamilifu mfumo na mabadiliko ya kisera na motisha ambayo ni muhimu kwa ajili ya kusukuma mbele maendeleo. Mikakati iliyowekwa ni ile iliyosisitiza mfumo wa Serikali kumiliki njia kuu za uzalishaji, ubadilishanaji na usambazaji kwa matarajio ya kuimarisha sekta ya umma (kwa sekta ya umma kupanua uwekezaji) kama ndio kichocheo cha ukuaji na maendeleo ya uchumi.

Licha ya kasoro kadhaa katika mikakati hii, Azimio la Arusha lilikusudiwa kujenga jamii yenye kudumisha mila, desturi, silka na maadili ya kijamii yanayokwenda na wakati. Hivyo, Tanzania hivi leo inajivunia na inafaidi kuwepo kwa umoja wa kitaifa, mshikamano, amani na utulivu wa kijamii vyote hivi vikiwa ni matokeo ya misingi mikuu ya Azimio la Arusha. Misingi hii haina budi ienziwe na kuchukuliwa kama ni sehemu ya nguzo muhimu katika utekelezaji wa Dira ya 2025.

## 2.2 Kasoro na Vikwazo

Maudhui makuu ya dira mbili za awali, kama ilivyobainishwa katika mipango mbali mbali ya maendeleo, ni azma ya kufikia mafanikio makubwa katika kuinua hali ya maisha ya watu. Hususan, Tanzania ilidhamiria kutokomeza umaskini, ujinga na maradhi. Ijapokuwa kuna mafanikio ya kuridhisha yaliyofikiwa katika nyanja za elimu na afya, kuna wasi wasi kwamba viwango vya maendeleo vilivyofikiwa havilingani na matarajio.

Ukweli ni kwamba, katika kipindi cha miaka ya 1980 dalili za kufifia kwa baadhi ya mafanikio yaliyopatikana zilianza kudhihirika. Katika muktadha huu, sababu ambazo zimekuwa ni vikwazo katika utekelezaji wa malengo ya mipango na programu za maendeleo ni sharti zibainishwe ili kutafuta ufumbuzi wake na pia kutuwezesha kubuni mbinu mwafaka katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa siku za usoni. Sababu nne zifuatazo zimeweza kubainishwa kuwa ni vikwazo:-

- Hulka ya kutegemea wahisani na fikra zilizodumaa kimaendeleo;
- Uchumi dhaifu na uwezo mdogo wa kusimamia uchumi huo;
- Udhaifu katika utawala na usimamizi wa uzalishaji mali; na
- Mipangilio mibaya ya utekelezaji.

### *2.2.1 Hulka tegemezi na fikra zilizodumaa kimaendeleo*

Fikra za watu na viongozi wa Tanzania zilikuwa zimedumaa katika kutegemea wahisani, hali ambayo ilififisha juhudi na moyo wa kujituma na hivyo kushindwa kuyamiliki na kuyaongoza maendeleo yao. Hali hii haikuwa muafaka katika mahitaji ya kukabiliana na changamoto za kimaendeleo kwa heshima, kujiamini na dhamira ya dhati ya kufikia hayo kwa

kufanya kazi kwa juhudi na ujasiri. Mfumo wa elimu uliopo haukuandaliwa kwa lengo la kukabiliana na upungufu huo, na kuwawezesha kumiliki agenda ya maendeleo yao na kuwafanya wajiamini katika kufikia maamuzi kuhusu hatma ya nchi yao.

Matokeo ya hali hiyo ni kuwepo kwa mambo yafuatayo:-

- Tabia ya kutegemea misaada, kutojiamini na ukosefu wa ari ya kujituma: kupungua kwa uwezo wa kuzitumia kikamilifu nguvu kazi, rasilimali na maarifa ili kwa dhati kabisa kuweza kuzingatia njia mbali mbali za kutatua matatizo yetu ya kimaendeleo. Matokeo ya hali hii ni kushindwa kuutumia uwezo mkubwa tulionao kutuletea maendeleo;

- Fikra za wananchi na viongozi wa Tanzania hazithamini utendaji bora wa kazi, ustadi, na ubunifu, wala hazijaweza kujenga mazingira mazuri kwa mambo haya ya msingi kuweza kuchomoza. Kwa hiyo, kuna kila dalili za watu kukata tama, kukosa utamaduni wa uwajibikaji na moyo wa kujituma. Ubunifu, uadilifu, uvumbuzi na ustadi katika jamii umeshuka sana. Matokeo yake ni kushamiri kwa utamaduni wa kutamani kupata mafanikio "bila ya kufanya kazi" na hivyo kufifia kwa moyo wa kujituma na tabia ya kuthamini maendeleo ya jamii;

- Kiwango na ubora wa elimu uliofikiwa bado haukidhi mahitaji yanayozidi kukua kulingana na changamoto za kimaendeleo na hivyo elimu haisaidii sana katika kutoa

ufumbuzi wa matatizo yanayolikabili Taifa. Kwa hakika bado mfumo wa elimu haujaandaliwa kikamilifu ili utumike kama nyenzo ya kufanya mtu binafsi ajione kwamba ni sehemu ya jamii. Hali kadhalika, elimu hiyo haijawajenga watanzania katika stadi za biashara wala kuwapa uwezo wa kujiajiri wenyewe.

### 2.2.2 *Uchumi dhaifu na Uwezo mdogo wa Usimamizi wa Uchumi*

Uwezo wa kusimamia uchumi umekuwa hauendelezwi kulingana na mahitaji ya kujenga utangamano katika uchumi kwa ujumla na umekuwa haubadiliki kwa kasi inayotakiwa ili kwenda sawa na mabadiliko yanayotokea. Kwa jumla, pamekuwa na ukosefu wa utangamano katika uchumi. Mabadiliko ya sera kulingana na mahitaji yanafanyika taratibu. Hali hii inaonyesha udhaifu katika uwezo wa kutunga sera muafaka ili kukabiliana na mabadiliko ya mara kwa mara. Matokeo yake ni kujengeka kwa mazingira yasiyoleta utulivu wa uchumi, hali ambayo ni muhimu kwa kuvutia wawekezaji wa uhakika. Kama hiyo haitoshi, kumekuwepo na matumizi makubwa ya mamlaka ya dola katika kusimamia uchumi, hata katika maeneo ambayo si muhimu na hii imedhoofisha fursa ya kushirikisha uwezo ulio nje ya Serikali. Matumizi yaliyokithiri ya mamlaka na urasimu yamepunguza uwezekano wa kutumia nguvu za soko kufikia malengo ya kimaendeleo na matokeo yake uchumi umekuwa dhaifu.

Kwa jumla uchumi wa Tanzania unaakisi mambo yafuatayo:

- Mfumo wa uchumi umebaki kuwa ule ule bila mabadiliko. Kilimo, kama uti wa mgongo wa uchumi, kimeendelea kutegemea zaidi mvua na teknolojia duni. Kwa hiyo, tija katika sekta ya kilimo ni duni na isiyobashirika.

- Tija katika sekta nyingine pia ni ndogo. Rasilimali zilizopo hazijaweza kutumiwa ipasavyo katika kuchochea maendeleo ya haraka na endelevu. Kiwango hiki kidogo cha tija pia ni kielelezo cha kiwango kidogo cha ubunifu na ustadi katika jamii ikiwa ni pamoja na matumizi madogo ya sayansi na teknolojia.

- Mfumo wa uchumi kwa kiwango kikubwa umeendelea kutegemea uzalishaji wa malighafi, hivyo kuufanya uchumi mara kwa mara kuathiriwa sana na mabadiliko ya mara kwa mara katika masoko ya kimataifa na kuzidi kuvumbuliwa kwa teknolojia mpya zenye kutumia malighafi kidogo.

- Maendeleo yaliyopo, kwa jumla, yanadhihirisha kuwepo kwa matumizi madogo ya rasilimali asilia za nchi, nguvu kazi na hata fedha kwa ajili ya kukuza pato la Taifa na kuinua hali za maisha ya wananchi.

### *2.2.3 Udhaifu katika Utawala na usimamizi wa Maendeleo*

Kwa kipindi kirefu na hasa katika miaka ya karibuni, kumeanza

kujitokeza dalili za kupungua kwa mshikamano wa kijamii na umoja wa kitaifa. Rushwa na matendo mengine maovu katika jamii yamezidi kuongezeka. Hali hii ni ya hatari. Utawala wa sheria na nafasi ya watu katika maamuzi ya kimaendeleo inazidi kupungua. Taasisi za Kitaifa na mfumo wa uendeshaji haujafanyiwa marekebisho kulingana na mahitaji halisi ya mageuzi yanayoendelea. Matokeo yake, mfumo huu umekuwa hausaidii katika kuleta mahusiano mazuri ya kijamii, kuruhusu ushiriki mpana katika shughuli za maendeleo na mfumo huu hasa umeshindwa kukuza rasilimali na uwezo wa ndani kuweza kukabili changamoto zinazojitokeza katika mfumo wa soko huria na maendeleo yenye kuongozwa na sekta binafsi.

### *2.2.4 Utamaduni Mbovu wa Utekelezaji*

Watanzania wamejijengea sifa ya kutayarisha na kujitangazia mipango, programu na malengo ambayo mara nyingi yamekuwa hayana mpangilio mzuri wa utekelezaji, uratibu na taratibu za tathmini. Matokeo yake, utekelezaji umekuwa dhaifu. Hali hii imesababisha kupungua kwa imani na matumaini ya wananchi kwa viongozi wao. Ni dhahiri kwamba wananchi hivi sasa hawana hamasa ya kushiriki katika mipango ya kitaifa. Wananchi wamekata tamaa.

## 3.0 MALENGO YA DIRA

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ina malengo ya kuwaletea wananchi maisha bora na mazuri, kuwa na uongozi bora na utawala wa kicheria, na kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani. Inatarajiwa kwamba mafanikio yafuatayo yatafikiwa ifikapo mwaka 2025.

### 3.1 Maisha Bora na mazuri

Hali bora ya maisha kwa Watanzania wote inategemea kufikiwa kwa kutumia mikakati na sera ambazo zitawezesha kufikia malengo yafuatayo:-

- Kujitosheleza kwa chakula na kuwa na uhakika wa upatikanaji wake;

- Elimu ya msingi kwa wote, kufuta ujinga na kufikia kiwango kinachoridhisha cha elimu ya kati na juu kulingana na mahitaji ya kuwa na watenda kazi wenye uwezo wa kushughulikia kikamilifu changamoto za kimaendeleo katika ngazi zote;

- Usawa wa kijinsia na kuwapa fursa wanawake kushiriki kikamilifu katika masuala yote ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni;

- Upatikanaji wa huduma za msingi kwa watu wote;
- Upatikanaji wa huduma bora za uzazi kwa watu wote wenye umri unaostahili;
- Kupunguza vifo vya watoto wachanga na vifo vya uzazi kwa robo tatu ya viwango vya sasa;
- Upatikanaji wa maji salama kwa watu wote;
- Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kulingana na kiwango kilichofikiwa na nchi zenye mapato ya kati;
- Kuondoa kabisa umaskini uliokithiri.

## 3.2 Uongozi bora na utawala wa kisheria

Inakusudiwa kwamba jamii ya Watanzania itakuwa na sifa zifuatazo:-

- Maadili mema na kuthamini utamaduni;
- Uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria;
- Kutokuwepo rushwa na maovu mengine;
- Jamii iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na

uzoefu wake na wa wengine na yenye kumiliki na kubaini agenda ya maendeleo yake.

## 3.3 Uchumi Imara na wenye uwezo wa ushindani

Uchumi unatarajiwa uwe na sifa zifuatazo:

- Kuwa na vianzio mbalimbali vya uzalishaji na uchumi ambao una maendeleo ya viwanda yaliyo karibu sana na nchi zenye mapato ya kati;

- Utangamano wa uchumi unaojidhihirisha kwa kuwepo kwa kasi ndogo ya upandaji wa bei na uwiano madhubuti wa uchumi kwa jumla;

- Ukuaji wa uchumi kwa asilimia 8 au zaidi kwa mwaka;

- Kuwepo kwa miundombinu ya kutosha kuweza kukidhi mahitaji ya malengo ya Dira katika sekta zote;

- Mshiriki na mshindani shupavu katika masoko ya nchi jirani na ya dunia kwa jumla, ikiwa ni pamoja na kupanga na kuendeleza maslahi ya Taifa na kuwa na uwezo wa kujirekebisha haraka ili kuweza kukabili mabadiliko yanayotokea katika masoko ya nchi jirani na ya dunia.

Inatarajiwa pia kwamba ukuaji wa uchumi utakwenda sawia na urekebishaji wa hali ya sasa ya uharibifu wa mazingira na rasilimali (kama vile misitu, samaki, vianzio vya maji, hali ya hewa, udongo, na viumbe mbali mbali) ikiwa ni pamoja na kupunguza mlundikano wa vitu vyenye kuhatarisha maisha.

## 4.0 MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIWA KATIKA UTEKELEZAJI

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 itafanikiwa tu endapo Watanzania watakusanya na kutumia uwezo wao ipasavyo na kuzingatia mambo muhimu yatakayofanikisha utekelezaji wa Dira na pia kuepuka kabisa vikwazo vilivyowakwamisha huku nyuma. Mambo makuu ambayo Watanzania wanapaswa kuyazingatia ni umoja wa kitaifa, mshikamano wa kijamii, amani na utulivu. Hata hivyo, haya yote ambayo yamepatikana kutokana na misingi ya Azimio la Arusha, ni vyema yasihesabike kama yasiyoweza kutoweka. Mambo hayo yamejengeka katika muda mrefu na ndizo nguzo za matumaini na matarajio ya Watanzania walio wengi. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni, kuna dalili kuwa matumaini na matarajio hayo yameanza kufifia. Changamoto muhimu kwa sasa ni kuhakikisha kuwa juhudi za makusudi zinafanyika kurejesha upya matumaini, kujiamini, imani na ari miongoni mwa watu yaani wanawake, wanaume na wananchi wote kwa ujumla ili malengo yaliyobainishwa katika dira yafanikiwe, kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea.

Ni dhahiri kuwa uchumi wa dunia na uchumi wa Tanzania umebadilika kwa kiasi kikubwa tangu kuanzishwa kwa Azimio la Arusha. Watanzania kwa hiyo hawana budi kujirekebisha kulingana na mazingira hayo mapya. Hususan, ni muhimu

kuyatambua mabadiliko yafuatayo yaliyotokea katika uchumi kitaifa na duniani kwa jumla:-

- Kuzuka kwa mifumo inayotofautiana ya kisiasa na kiuchumi;

- Kubainika kuwepo kwa kasoro katika maendeleo yaliyopatikana kwa kusimamiwa na sekta ya umma na mfumo wa uchumi ulioongozwa kiutawala na kuwa na mipango ya jumla;

- Kutambulika kwa jitihada za watu na sekta binafsi kama kichocheo muhimu katika ujenzi wa msingi imara wa uzalishaji na ukuzaji uchumi;

- Majukumu ya dola katika utoaji wa huduma na hifadhi ya jamii yamebadilika kwa kuzingatia zaidi ufanisi, upunguzaji gharama za uendeshaji na kuinua ubora wa huduma hizo;

- Mabadiliko makubwa yanayotokea katika nyanja za kibiashara na teknolojia;

- Mahusiano ya uchumi kimataifa yamebadilika ambapo sasa yanaongozwa na vigezo vilivyotokea baada ya kumalizika kwa vita baridi duniani;

- Mtazamo wa kiuchumi kitaifa unabadilishwa kufuatia kuzidi

kuimarika kwa mahusiano ya uchumi wa kikanda na kimataifa na hivyo kuathiri mtazamo wa uchumi kitaifa.

Mabadiliko haya yamezua changamoto mpya ambazo zitahitaji misingi mipya na madhubuti itakayoiwezesha Tanzania kujikwamua kutoka katika hali ya kiwango cha chini cha maendeleo na kufikia kiwango cha nchi zenye mapato ya kati na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu kama kinachobainishwa na ubora wa maisha ya watu wake. Kwa maana hii vichocheo vitatu vifuatavyo ni muhimu vikakuzwa na kutumiwa:-

- Fikra za kimaendeleo zenye kuambatana na hali ya kujiamini, uwajibikaji na kuthamini mila na desturi zenye kuwapatia watu fursa zaidi;
- Ustadi wa kazi na ari ya ushindani; na
- Uongozi bora na utawala wa kisheria.

## 4.1 Fikra za kimaendeleo na Utamaduni wa kujitegemea

Umuhimu mkubwa hauna budi uelekezwe kwenye masuala ya elimu na kujiendeleza. Sambamba na hilo, pana haja ya kuchukua hatua za makusudi kubadili fikra na desturi za watu ili zimwezeshe mtu binafsi na jamii kwa jumla kuendelea na kujenga jamii yenye kuweza kukabiliana na changamoto za

kimaendeleo na kuweza kutumia kila fursa inayopatikana kwa ajili ya kuboresha hali za maisha. Umilikaji thabiti wa agenda ya maendeleo ukiambatana na ujenzi wa moyo wa kujitegemea katika ngazi zote za kijamii ni masuala ya msingi ili kufanikisha utekelezaji wa Dira. Watanzania wanapaswa kujifunza kuheshimu na kuthamini uhodari wa kazi, ubunifu, utaalamu na ustadi wa kibiashara na wajizatiti kujenga utamaduni wa kuweka akiba na kuwekeza.

Mambo muhimu kuhusiana na kujenga fikra za kimaendeleo na utamaduni unaotoa fursa zaidi ni haya yafuatayo:

*i) Utamaduni wenye kuthamini uhodari wa kazi na Ubunifu*

Utamaduni wa kupenda maendeleo unahitaji kulelewa na kukuzwa katika shughuli zote za maisha ya watu kwa lengo la kufanikisha Dira na hasa kwa kutilia mkazo ujenzi wa ustadi wa kibiashara na kuwezesha mtu binafsi kujipatia maendeleo kwa kuongeza ubunifu, bidii ya kazi, ustadi, kuwajibika, kuthamini maisha, elimu, kuweka akiba na kuwekeza, na kukuza hali ya kujiamini na kujiheshimu.

*(ii) Utamaduni wa Kuweka Akiba na Kuwekeza*

Utamaduni na tabia ya kujiwekea akiba na kuwekeza katika maeneo yenye tija kwa lengo la kujenga utajiri kwa mtu binafsi, familia, jumuia na Taifa inatakiwa kujengwa na kuendelezwa. Kwa ajili hiyo hiyo, utamaduni wa kujenga utajiri na

kulimbikiza kwa ajili ya maendeleo unapaswa kukuzwa, ikiwa ni pamoja na kujenga utamaduni wa kuhifadhi na kufanyia matengenezo rasilimali iliyopo na kuzuia uharibifu usio wa lazima.

*iii) Ari ya Maendeleo ya Jumuiya*

Ari ya kimaendeleo ya Jumuiya inayowiana na bidii ya mtu binafsi katika kuinua na kusimamia shughuli za kijamii na kiuchumi na katika masuala mengine ya kitaifa, katika ngazi zote za jamii, inapaswa kukuzwa kwa kupandikiza utamaduni wa kuchangia na kubadilishana mawazo na nyenzo mbalimbali katika jumuiya na baina ya jumuiya moja na nyingine kama njia mojawapo ya kukusanya pamoja rasilimali kwa manufaa ya watu wote.

iv) *Mikakati ya Maendeleo ya watu*

Kuna haja ya kuwa na mikakati yenye wigo mpana ya uwekezaji katika maendeleo ya watu, itakayohusisha watu binafsi, familia, jumuiya, na mashirika mbalimbali katika kukusanya rasilimali kwa ajili hiyo.

v) *Jamii yenye kujifunza*

Jamii haina budi kuhimizwa na kuhamasishwa kujiendeleza ili iweze kuinua na kuboresha uwezo wake wa kukabiliana na vikwazo na pia kutumia fursa zinazopatikana kwa ajili ya maendeleo yake na kuboresha hali ya maisha.

vi) *Mfumo wa motisha unaozingatia ubora, ubunifu na ustadi*

Mfumo wa uendeshaji katika ngazi zote hauna budi kubadilishwa. Hii inawezekana kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa motisha kwa wananchi, makundi ya watu na makampuni kwa lengo la kuhamasisha maendeleo ya ubunifu, ustadi, uvumbuzi na ubora. Mageuzi haya yanapaswa kuwa wazi katika mfumo wa elimu, taasisi za mafunzo, ajira na upandishaji wa vyeo na katika utamaduni mzima wa uendeshaji biashara.

viii) *Elimu kama mbinu maalum ya kuleta mabadiliko*

Elimu inapaswa kuchukuliwa kama silaha muhimu katika mkakati wa kubadili fikra na kujenga taifa bora lililoelimika, lililojizatiti barabara kwa kuwa na maarifa yanayohitajika kuweza kukabiliana kwa ushupavu na werevu mkubwa na changamoto na taifa. Kwa hali hiyo, mfumo wa elimu unapaswa kubadilishwa na kuboreshwa zaidi kwa lengo la kukuza ubunifu na mbinu za kutatua matatizo.

## 4.2 Ustadi na Uwezo wa Ushindani Kiuchumi

Ustadi wa taifa katika kusimamia maendeleo utapatikana endapo Serikali itaweka mazingira muafaka kwa wahusika kutumia vizuri rasilimali za ndani ili kuwa na ushindani katika sekta mbali mbali za uchumi. Ustadi na uwezo wa ushindani kama suala muhimu la kufanikisha utekelezaji litafanikiwa tu endapo tutakuwepo na mazingira mazuri ya usimamizi wa uchumi,

miundo mbinu bora na ya kutosha, elimu bora, utumiaji mkubwa wa rasilimali za ndani, kukuza uzalishaji na kuongeza uwezo wa kukabiliana ipasavyo na mabadiliko ya nje.

Baadhi ya mikakati kwa ajili ya kufanikisha lengo hili ni kama ifuatayo:

i) *Sera bora za kuongoza uchumi*

Umuhimu wa kuyatafsiri upya majukumu ya Serikali na kuinua uwezo wake wa kuongoza uchumi kupitia sera unahitaji kupewa kipaumbele. Lengo ni kuhakikisha kuwepo kwa utangamano, uendelevu na mazingira ya uchumi yanayobashirika. Kwa hiyo, pana haja ya kuweka mazingira sahihi na imara ya uchumi kitaifa kwa kutambua kuwepo kwa sera sahihi za kiuchumi zenye kuwezesha kufikia viwango vikubwa vya ulimbikizaji na uwekezaji; kudumisha utangamano wa bei na kujenga uwiano mzuri wa mizania ya uchumi ili kuhakikisha kwamba jamii ya Watanzania haiishi nje ya uwezo wake.

ii) *Maendeleo ya Miundombinu*

Uwekezaji katika miundombinu ni lazima upewe kipaumbele, na Serikali inatakiwa kuwa mstari wa mbele katika suala hili. Uwekezaji huu pia unapaswa kuihusisha sekta binafsi na jamii kwa jumla. Ujenzi wa mtandao mzuri wa barabara ni muhimu katika kuleta maendeleo vijijini. Uwekezaji katika nishati, maji na mawasiliano ni kivutio muhimu kwa wawekezaji wa ndani na nje ili kuinua mapato na kupanua ajira.

iii) *Ukuzaji wa Elimu ya Sayansi na Teknolojia*

Mfumo wa Elimu sharti ujenge utamaduni wa matumizi ya sayansi na teknolojia kuanzia katika ngazi za chini, kwa kuwapatia watoto wa umri kati ya miaka 6 na 15 elimu iliyo bora. Sayansi ya msingi na hisabati ni masomo ambayo hayana budi kupewa umuhimu ili kwenda sambamba na mahitaji ya enzi hii ya teknolojia. Elimu ya Sayansi na Teknolojia na ufahamu kuhusu matumizi yake katika kuinua na kukuza tija sharti ifike kwenye jamii nzima kwa kuanzisha kampeni za uhamasishaji wa wananchi kujiendeleza.

iv) *Ukuzaji wa Teknolojia ya Upashanaji Habari na Mawasiliano*

Teknolojia za upashanaji habari na mawasiliano ni muhimu katika kuleta mageuzi ya kijamii na kiuchumi. Gharama ya teknolojia hii inaendelea kupungua siku hata siku wakati uwezo wake na tija yake vinazidi kuongezeka. Teknolojia hizi ni muhimu sana katika kufanikisha malengo ya Dira. Kwa hiyo zinapaswa kuendelezwa katika sekta zote za uchumi na kutumiwa kwa manufaa ya makundi yote katika jamii kwa lengo la kuiwezesha jamii kujipatia mahitaji yake muhimu, kuongeza tija na kujenga uwezo wake wa ushindani. Fursa mpya zinazozidi kutokea kufuatia maendeleo ya teknolojia za upashanaji habari na mawasiliano zinaweza kutumika vyema kufikia malengo ya Dira. Hata hivyo, ujuzi sahihi na vipaji mahsusi vinahitajika kwa ajili ya maendeleo hayo. Dhima hii inahitaji uwekezaji wa rasilimali ya kutosha ili kuboresha elimu

yenye msingi madhubuti wa sayansi na kujenga taifa lililoelimika.

v) *Matumizi ya Rasilimali za ndani*

Ukusanyaji na utumiaji mzuri wa rasilimali za nchi (maliasili, fedha na watu) ni muhimu na ni msingi ambao utekelezaji wa Dira utategemea. Rasilimali hizi sharti zitumike kujenga uwezo wa kuendeleza shughuli za kiuchumi hasa zenye fursa ya kuinua uwezo wa ushindani na kumudu athari za mabadiliko ya uchumi kutoka nchi za nje .

vi) *Mapinduzi ya kiuchumi ili kuinua ushindani*

Ubora wa hali za maisha hauna budi ukuzwe kwa kuinua tija katika sekta zote. Lengo hili litafikiwa kwa kuubadili uchumi kuwa imara, usioyumba na wenye kuhimili ushindani na wenye msingi madhubuti wa sayansi na teknolojia. Mkakati utakaotumiwa ni ule wa kubadilisha mfumo wa kiuchumi kutuwezesha kuondokana na uchumi unaotegemea kilimo cha jadi chenye kiwango duni cha tija na kujenga uchumi wenye mawanda mapana, wenye maendeleo ya kati ya viwanda sawia na maendelkeo ya kisasa vijijini kuweza kuwa na tija kubwa katika sekta ya kilimo, kuinua mapato na kuhakikisha upatikanaji na kujitosheleza kwa chakula.Uchumi wenye vyanzo mbalimbali msingi wake sharti utokane na program za kuendeleza kekta ya viwanda iliyoelekezwa kutumia zaidi rasilimali za ndani (hasa viwanda vinavyotumia bidhaa za kilimo) na yenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya sekta nyingine na kuendeleza fursa zaidi kwa ushindani.

*vii). Kujenga uwezo wa kukabiliana na kubashiri mabadiliko ya nje*

Uwezo wa kubashiri na kukabiliana ipasavyo na mabadiliko ya nje unapaswa kujengwa kama jambo muhimu ili kuweza kujizatiti katika masoko ya dunia yenye kubadilika mara kwa mara, mwelekeo wa kiteknolojia na mabadiliko katika hali ya mazingira .Kipaumbele sharti kiwekwe katika kujenga uwezo wa kujifunza na kuwa wabunifu katika kukabiliana na changamoto za asili na matukio ya kiuchumi yanayotokea katika nchi za jirani na duniani.

## 4.3 Uongozi bora na utawala wa kisheria

Uongozi sharti ufanywe kuwa zana muhimu katika kuleta maendeleo, usawa, umoja na amani inayotokana na kuheshimu utawala wa kisheria na ushirikishwaji wa umma katika vita dhidi ya rushwa na maovu mengine katika jamii. Uongozi bora unapaswa kuwa ni sehemu ya mfumo wa jamii, uratibu na mahusiano katika harakati za maendeleo. Hali hii inaweza kufikiwa kwa kuweka mfumo wa taasisi wenye uwezo wa kuunganisha sifa zote nzuri na kuratibu juhudi zote za maendeleo katika jamii. Uongozi bora sharti ujengwe kwa kukuza utamaduni wa uwajibikaji na kuonyesha wazi mfumo wa motisha kulingana na utendaji mzuri na mfumo wa utoaji adhabu.

Mfumo sahihi wa taasisi unahitajika kwa kuhamasisha ari ya wanawake, wanaume na vijana kuwa wabunifu. Hii ni pamoja na

kuainisha juhudi mbalimbali, kwa kutambua na kuzitunukia juhudi kadri zinavyostahili. Mfumo huu unahitaji nguzo tatu muhimu:-

*i) Kutambua na kutumia nguvu ya soko na sekta binafsi*

Kutumia nguvu ya soko na jitihada za watu binafsi katika kufikia kiwango cha juu cha ukuzaji wa uchumi.

*ii) Kuweka uwiano mwafaka baina ya dola na taasisi nyingine.*

Majukumu ya Serikali na nafasi yake mpya katika uchumi sharti yawekwe bayana ili kutoa nafasi na kuainisha majukumu ya taasisi mbalimbali (k.m familia, vitengo vya kibiashara na jumuia za kiraia) kushiriki katika soko kwa kuzingatia hali ya kitaifa na kidunia.

Majukumu maalum ya Serikali yatakuwa ni:-

- Kuhakikisha kuwepo kwa mfumo bora wa sheria na usimamizi mzuri;
- Kushiriki moja kwa moja na kuhamasisha washiriki wengine kuwekeza rasilimali katika maendeleo ya miundombinu;
- Kushiriki moja kwa moja na kuhamasisha washiriki wengine kuwekeza rasilimali katika maendeleo ya elimu na mafunzo;

- Kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi na uwajibikaji katika kujenga uwezo wa dola kusaidia na kusimamia shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya makusudi kuweza kuvutia wawekezaji katika maeneo maalumu na kusaidia viwanda teule;

- Kuhakikisha kwamba mfumo wa soko unaruhusu ushiriki mpana kwa wanaume, wanawake, vijana na wananchi kwa jumla katika shughuli zenye kulenga kufanikisha Dira. Serikali itapaswa kuweka mipango madhubuti kwa lengo la kukuza ushiriki wa wananchi wazawa katika mustakabali wa kuendeleza na kumiliki uchumi. Programu hizi ni sharti zisaidiwe ipasavyo kuhakikisha kwamba nafasi ya Watanzania katika kumiliki na kuendesha uchumi inaimarika; na

- Kuhakikisha kwamba utaratibu wa kukusanya maoni, kushauriana na kujenga mtandao wa ushirikiano baina ya wahusika mbalimbali katika uchumi umejengwa na unafanya kazi iliyokusudiwa.

*iii)* *Kukuza ushirikishwaji wa kidemokrasia*

Juhudi za makusudi sharti zifanywe kuwapa wananchi uwezo wa kushiriki katika kufikia maamuzi kidemokrasia. Mkakati uhusishe kutoa mamlaka na madaraka zaidi kwa Serikali za Mitaa na jumuiya za wananchi na kusaidia kukuza ushiriki wao katika kukusanya rasilimali na kuunganisha ujuzi na maarifa kwa lengo la kuchochea juhudi katika ngazi mbalimbali za jamii.

# 5.0 UTEKELEZAJI WA DIRA

## UTEKELEZAJI WA DIRA

Mafanikio dhahiri ya Dira ya Maendeleo 2025 yatategemea utekelezaji wake. Mambo mawili ni muhimu kabisa yawepo ili kuwa na mafanikio katika utekelezaji wa Dira ya maendeleo 2025. Mambo hayo ni uongozi bora na uchumi imara. Ni wazi kwamba mambo hayo hayawezi kuibuka ghafla. Inabidi yatokane na juhudi au hatua za makusudi. Ikitokea (kwa mfano) kwamba yote yakakosekana, kipindi chote hadi mwaka 2025 kinaweza kisionyeshe mabadiliko yeyote katika maisha ya wananchi, isipokuwa hali inaweza kuwa mbaya zaidi mwaka hadi mwaka. Kama kutakuwepo na uongozi bora lakini uchumi ukawa dhaifu au kukawa na uchumi imara lakini uongozi ukawa dhaifu, kunaweza kukawapo mafanikio kiasi wakati fulani, lakini kwa vyovyote vile mafanikio hayo hayawezi yakadumu kwa hiyo hayawezi kubadilisha kwa kiasi kikubwa maisha ya wananchi. Uchumi hauwezi kuendelea kuwa imara kwa muda mrefu ikiwa uongozi unalegalega na ubora wa uongozi hautaweza kuonekana kama uchumi unazama. Mafanikio ya kudumu ya Dira ya maendeleo ya Tanzania 2025 hayana budi yatokane na uongozi bora sambamba na ujenzi wa uchumi imara.

Uzoefu wa Tanzania unadhihirisha wazi umuhimu wa uongozi katika suala zima la maendeleo. Azimio la Arusha lilipotangazwa, suala la uongozi bora ni mojawapo ya mambo yaliyoainishwa kuwa muhimu katika kuleta maendeleo

yanayolingana na mtazamo wa Azimio hilo. Sera mbalimbali zilizolenga kwenye kuleta mabadiliko katika hali ya wananch zilitungwa na kulifanyika uhamasishaji mkubwa wa wananchi katika kuzitekeleza. Aidha, mipango ya kuongeza uwezo au ujuzi wa watendaji katika maeneo mbalimbali iliandaliwa na kutekelezwa.

Sawa na ilivyokua kwa Azimio la Arusha, uongozi bora ni suala muhimu katika kufanikisha Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025. Ni muhimu uongozi uwe fikra pevu za kimaendeleo na utoe tafsiri ya fikra hizo katika utendaji wake wa kila siku . Ni muhimu vile vile uongozi uwe na uwezo wa kujenga na kuhakikisha kuwepo kwa mfumo wa utawala unaoweza kusimamia na kuratibu utekelezaji kwa kinaganaga.
Aidha, panahitajika uongozi ambao daima upo tayari kujifunza na kusikiliza ushauri mbalimbali na kwa jumla unatakiwa uongozi ambao upo karibu na jamii. Taratibu za kuelekeza uongozi kwenye mtazamo wa namna hiyo inabidi ziandaliwe au (katika nyanja au maeneo ambapo tayari zimeshaanza) ziimarishwe. Pamoja na kukuza ustadi wao, itabidi watendaji katika ngazi mbalimbali wawe sambamba na viongozi katika mtazamo wao pia.

Upo uhusiano wa karibu sana baina ya hali ya maisha ya wananchi, jamii na mtu binafsi na uwezo wa uchumi kutoa mahitaji yanayomwezesha mtu, jamii na wananchi kuishi na kustawi. Tanzania inao uzoefu katika suala hili vile vile. Hadi

katikati ya miaka ya 1970, uchumi uliweza kukua kwa wastani wa asilimia 5 – 6 kwa mwaka na viwango vya upandaji wa bei vilikua vidogo. Nafuu iliyokuwepo katika maisha ya wananchi wakati huo ilitokana na hali hiyo. Kutoendelea kuwepo kwa hali hiyo katika miaka iliyofuata ni matokeo ya vurugu yaliyotokea katika uchumi, na hivyo uchumi ukashindwa kukimu matakwa ya mwananchi pamoja na kwamba ulikua anuai zaidi ikilinganishwa na miaka ya 1960 na 1970. Uchumi ulianza kuyumba, hali ambayo ilionekana katika ukuaji mdogo na viwango vikubwa vya upandaji bei.

Ili kuweza kurejea na kuvuka hali iliyokuwepo miaka ya 1960 na 1970, uchumi imara na unaokua kwa kiwango kikubwa ni muhimu sana. Panahitajika kuwepo kwa uchumi wenye uwezo wa kukabili na kuweza kunufaika na ushindani unaoongezeka. Viongozi na watendaji sharti wabainishe mikakati na mbinu za kuwezesha kuwepo kwa uchumi wa namna hiyo.

Kwa jumla, utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 unapashwa kuchochea mambo yafuatayo:-

*i)* *Fikra za kimaendeleo na ari ya ushindani*

Jamii ili iweze kufikia hali hii, pana haja ya:-

- Kuhakikisha usimamizi imara wa uchumi;
- Kuendeleza uwekezaji katika kuimarisha miundombinu kwa kujumuisha Serikali, sekta binafsi na jumuiya mbalimbali za wananchi;
- Kuamsha upya ari ya kujitegemea na juhudi za kutafuta mali na kuweka akiba ili kupunguza na kumaliza tatizo la kutegemea wafadhili, hali ambayo imepelekea Watanzania

wengi kubweteka;

- Kufanya marekebisho katika mfumo wa elimu na kuendeleza rasilimali ya watu kulingana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yanayotarajiwa kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025. Mitaala ya Elimu mashuleni sharti irekebishwe kulingana na mahitaji ya utekelezaji wa Dira ya mwaka 2025.

*ii) Demokrasia na Ushirikishwaji wa Umma*

Ili kufikia hali hii, jamii yetu haina budi:-

- Kujenga jamii yenye kuthamini uwazi na Demokrasia na inayotoa fursa kwa watu wote. Hii inahitaji kuwepo kwa mwamko na welekevu halisi wa jamii kushiriki katika kupambanua mahitaji na matarajio yao pamoja na kujivunia utekelezaji wajibu wa kijamii.
- Kuhamasisha jamii kutumia mfumo uliopo wa kidemokrasia kuweza kuchagua viongozi bora, wasio wala rushwa na wawajibikaji. Viongozi sharti pia wawe waadilifu, wakereketwa wa maendeleo ya jamii na wenye dhamira ya kukidhi matakwa na mahitaji ya umma.
- Kuongeza ufanisi katika utoji wa huduma kwa umma kwa kuhakikisha watumishi wa serikali wanawajibika kwa wananchi.

- Kutoa fursa kubwa kwa wananchi kushika hatamu katika kusimamia maendeleo. Wananchi ndio wanaoelewa vizuri mahitaji yao na wana fursa nzuri zaidi ya kuamua juu ya matatizo yapi yanaweza kupatiwa ufumbuzi na kwa njia zipi.

- Kuwapa wananchi mamlaka zaidi ya kufanya maamuzi, kupanga na kusimamia mapato na kuweka mfano unaohakikisha uwajibikaji kwa mtu binafsi, familia, jumuiya na serikali za mitaa katika kufikia malengo ya jumla ya Dira.

*iii) Mfumo sahihi wa uratibu, tathmini, mapitio*

Mfano huu ni muhimu ili :-

- Kuhakikisha kwamba kazi ya kuratibu na kutathmini inafanyika ipasavyo kwa lengo la kubainisha ufanisi katika utekelezaji wa Malengo ya Dira ya 2025. Njia bora ya ufuatiliaji wa utekelezaji huo ni kuanza kwa kupambanua matarajio yaliyopangwa na baadaye kurudi nyuma na kuweka vigezo halisi vya utekelezaji.

- Kubainisha vigezo mahususi na vinavyopimika vitakavyosaidia katika kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Dira.

- Kuifanyia Dira mapitio kila baada ya miaka mitano ili kuweza kupima mafanikio ya Taifa na kubainisha marekebisho yanayohitajika katika sehemu ya tathmini na ufuatiliaji.

- Kuanzisha mfumo madhubuti wa uenezaji wa habari na mawasiliano ili kufanikisha kufanyika kwa uratibu na tathmini katika muda unaotakiwa na kuhakikisha kuwepo kwa mshikamano baina ya washiriki mbali mbali katika jamii.

*iv) Uongozi na utawala wa kisheria*

Kuwepo kwa hali hii kunaitaka jamii.

- Kujenga uwezo wa sekta ya Umma,taasisi za kijamii, vyombo vya habari, bunge, taasisi za kusimamia sheria na taasisi zote za ndani na nje ya dola zenye kuweza kuchochea uwajibikaji na kutetea matakwa ya jamii.

- Kuhamasisha watu waweze kuongeza uelewa wao kwa kuzingatia mahitaji ya utekelezaji wa Dira.

- Kuweka mikakati ya kujenga uadilifu, uwajibikaji na uwazi.

- Kuhakikisha kwamba taasisi zote zinazotoa huduma zinatoa taarifa na mchanganuo wa kweli na sahihi kuhusu utoaji huduma kwa umma.

- Kubainisha na kusimika nguzo na maadili ya Dira katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ili kuifanya ienziwe na kufuatwa na hivyo kuwaunganisha Watanzania katika kufanikisha utekelezaji wa Dira kwa kipindi chote.

## 6.0 HITIMISHO

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inalenga katika kukuza uzalendo na utaifa na pia kuimarisha mshikamano wa watu wote nchini, kwa kuzingatia mazingira ya sasa ya kiuchumi, kisiasa, itikadi n.k. Mshikamano wa Kitaifa utaweza kufikiwa ikiwa utekezaji wa Dira utatoa fursa kwa watu wote na kuwashirikisha katika kufaidi matunda yake. Utayarishaji wa Dira umekamilishwa kwa muafaka baada ya kuyashirikisha makundi mbali mbali katika jamii kwa mifumo ya kongamano, usaili, mikutano n.k. Inasisitizwa kwamba utekelezaji wa Dira pia utumie mfumo wa ushirikishaji. Ni kwa njia hiyo tu ya ushirikishaji ndipo Dira itazingatia maendeleo ya watu na kusimamiwa na watu wenyewe, vitu ambavyo ni vya msingi katika kuwafanya wananchi wawe na wajibu katika kufanikisha malengo yao.

Imetolewa na: Ofisi ya Rais
Tume Ya Mipango
Dar es Salaam
1999

Kimepigwa Chapa na Kiwanda cha Uchapaji cha Wizara ya Elimu Press "A"
S.L.P 9121, Simu: +255 22 2110692, Br. ya Magogoni, DAR ES SALAAM.